**Taarifa kwa Vyombo vya Habari**
**Imetolewa14 Mei 2013, saa 5 asubuhi**

# Wazazi wazungumzia matokeo ya Kidato cha 4

## Watupa lawama kwa serikali na walimu kuhusu ongezeko la wanafunzi kufeli mitihani

**14 Mei 2013, Dar es Salaam:** Wazazi wana ufahamu kuhusu mwendelezo wa kuanguka kwa ubora wa elimu ya sekondari, na kwa kiasi kikubwa wanatupa lawama kwa serikali na walimu kwa kuanguka huko. Wazazi wanaitaka serikali kuongeza idadi ya walimu waliofuzu na wenye sifa stahiki na wanaolipwa vizuri iliwasaidie kuboresha elimu nchini Tanzania.

Matokeo haya yamechapishwa katika muhtasari wa Twaweza unaoitwa *Matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Nne: Wananchi wazungumzia mgogoro wa kujifunza Tanzania*. Muhtasari huo umeandaliwa kutokana na takwimu zilizokusanywa kupitia utafiti wa *Sauti za Wananchi*, ambao ni utafiti wa njia ya simu za mkononi wenye sura ya uwakilishi wa kaya kitaifa kote Tanzania Bara. Wahojiwa waliombwa kueleza maoni yao kuhusu elimu, na kubaini changamoto na njia za kuongeza ubora. Takwimu zilizotumika kwenye Muhtasari huu zilikusanywa kati ya tarehe 18 Machi hadi 3 Aprili, 2013 kabla ya tangazo la serikali la kurekebisha matokeo ya Kidato Cha Nne ya mwaka 2012.

Miongoni mwa waliohojiwa, asilimia 68 ya wananchi walikuwa na taarifa kwamba matokeo ya Mitihani ya Kidato cha Nne ya 2012 yalikuwa yamechapishwa. Idadi kubwa ya wahojiwa walionesha kutambua kuanguka kwa ubora wa elimu ya sekondari katika miaka kumi iliyopita, ambapo wananchi asilimia 83 walionesha kwamba elimu ilikuwa imeporomoka. Idadi hiyo inaendana na takwimu rasmi zikiwamo zile za Wizara ya Elimu zinazojulikana kama Basic Education Statistics in Tanzania (BEST).

Walipododoswa zaidi, wazazi waliripoti kuhusu upungufu wa vitabu vya kiada kwa watoto wao. Katika ngazi ya shule za msingi, asilimia 55 ya wazazi waliripoti kwamba watoto wao hawakuwa na vitabu vya kiada; katika ngazi ya sekondari, asilimia 54 ya wazazi waliripoti kwamba watoto wao wana walau vitabu viwili vya kiada. Hata hivyo, wanafunzi wa sekondari wanatarajiwa wawe na walau kitabu kimoja cha kiada kwa kila somo, ambapo wana masomo kati ya sita hadi tisa. Licha ya ukweli huu, wazazi walipoulizwa kubaini vikwazo vikuu kwa ufaulu wa watoto wao kwenye mitihani, asilimia 3 tuu ya wazazi walitaja suala la ukosefu wa vitendea kazi shuleni.

Twaweza inaamini kwamba wazazi wanaojituma na kushirikishwa wanaweza kusaidia kukuza ubora wa viwango vya kujifunza vya watoto. Walipotakiwa kubaini nani alihusika zaidi na matokeo mabaya ya hivi karibuni, walisema pia kuwa wazazi wenyewe wanahusika, lakini walitajwa na asilimia 3 tu ya wahojiwa. Zaidi ya hilo, walipoulizwa kuhusu viwango vya ushiriki wao katika elimu ya watoto, wengi walijibu wanashiriki. Asilimia 64 ya wazazi waliripoti kukagua madaftari ya watoto wao katika wiki moja kabla ya utafiti, wengine asilimia 41 waliripoti kuwasaidia watoto kufanya kazi zao za ziada za masomo katika kipindi hicho hicho.

Wazazi wenyewe kwa kiasi kikubwa waliwalenga walimu na masuala mengine yanayohusiana kama sababu kuu ya matokeo mabaya ya hivi karibuni, na kwamba wao ndiyo walio muhimu katika kuboresha elimu. Zaidi ya nusu ya wazazi waliohojiwa walipendekeza kwamba, ili kuboresha mfumo wa elimu,

serikali inapaswa kuongeza idadi ya walimu, umahiri wa walimu na mishahara na kuhakikisha kwamba walimu wanalipwa kwa wakati. Suala hili liliendana na vikwazo vilivyotajwa na wazazi kuhusu ufaulu wa watoto kwenye mitihani. Kwa wastani, asilimia 54 ya wazaziwenye watoto katika shule za msingi na sekondari walitaja ari na motisha ndogo ya walimu, sifa duni za walimu na upungufu wa walimu ndiyo sababu. Kwa namna inayoshabihiana na hiyo, asilimia 34 ya wazazi waliwalaumu walimu kwa matokeo mabaya ya mitihani ya hivi karibuni, pia asilimia 38 ya wazazi waliitupia serikali lawama.

Elvis Mushi, Mtafiti wa Twaweza, alitoa maoni kuhusu matokeo hayo: *"Wazazi wanaelewa bayana kwamba mfumo wa elimu unawaangusha watoto wao. Kwa upande wao wanajibidiisha kushiriki katika elimu ya watoto wao na wanawataka walimu na serikali kutimiza wajibu wao."*

Jambo zuri lililotokana na kuchapishwa kwa Matokeo ya Kidato cha Nne 2012 ni kwamba limeibua mjadala wa kitaifa unaowahusisha wananchi, vyombo vya habari na duru za sera, kuhusu hali ya elimu Tanzania. Muhtasari huu unatoa takwimu za hivi karibuni zenye sura ya uwakilishi wa kitaifa na maoni ya wananchi kuhusu elimu katika mjadala huu.

Rakesh Rajani, Mkuu wa Twaweza, alisema *"Kupitia Sauti za Wananchi tunaweza kusikia kwa mara moja na kwa njia za kisayansi maoni ya wananchi kuhusu masuala yanayoathiri maisha yao. Wazazi wamezungumza wazi wazi kuhusu matokeo ya hivi karibuni ya Kidato cha Nne. Kwa mtazamo wao, ni wazi kwamba kuwahamasisha na kuwafanya walimu wawajibike ndiyo ufunguo wa kuongeza ubora wa elimu nchini."*

**---- Mwisho ----**

**Kwa taarifa zaidi:**
Risha Chande
Meneja wa Mawasiliano, Twaweza
Baruapepe: rchande@twaweza.org | Simu: (+255) (0) 656 657 559

**Matini kwa Wahariri**

- Takwimu kamili za utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 1 kuhusu matokeo ya mtihani wa kidato cha nne unaweza kupatikana kupitia www.twaweza.org/sauti
- Twaweza ni mpango wa miaka kumi unaolenga kuleta mabadiliko makubwa katika Afrika Mashariki. Twaweza ina-amini kwamba mabadiliko ya kudumu yanahitaji kutoka kwa wananchi wenyewe "bottom-up", na inajishughulisha kuendeleza hali na kupanua fursa ambazo kwa kupitia hizo mamilioni ya watu wanaweza kupata habari na kuleta mabadiliko katika jamii zao moja kwa moja na kwa kuiwajibisha serikali.
- Uwazi iliyoko Twaweza inatoa na kusambaza takwimu na taarifa muhimu ili kufahamisha mijadala ya umma. Dhamira ya Uwazi ni kuwawezesha walengwa wakuu kupata taarifa za kuaminika, kwa wakati, na chambuzi zinazoeleweka kwa urahisi ili kuboresha mijadala ya umma na kuchangia katika kuinua uwajibikaji na ushiriki wa wananchi.
- Unaweza kufuatilia kazi za Twaweza kwenye
  **Tovuti:** www.twaweza.org **Ukurasa wa Facebook:** Twaweza Tanzania
  **Anwani ya Twitter:** @Twaweza_NiSisi